**MASOMO YA WAKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA**

## DHAMBI NA MATOKEO YAKE (SEHEMU YA 1)

**SOMO:** Mwanzo 2 na 3

Dunia iko katika hali mbaya: vita, njaa, magonjwa, vurugu, mauaji, mateso n.k. Lakini, Mungu aliiumba dunia ikiwa ‘njema’. Ni mwanadamu aliyeichafua! Hulka ya mwanadamu ya uchoyo, ubinafsi, wivu na kutotii-mamlaka vimeiharibu jamii na dunia hii.

### Yalianzia wapi ‘kwenda mrama’?

Hapo mwanzo Mungu alimuumba mwanadamu wa kwanza, Adamu. Adamu aliumbwa kutokana na mavumbi ya nchi:

> “Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya nchi, akampulizia puani pumzi ya uhai, mtu akawa nafsi hai” (Mwanzo 2:7).

Mungu aliweka bustani nzuri kwa ajili ya Adamu kuishi humo, na baada ya hapo akampatia mke aliyemwita Hawa. Adamu na Hawa hawakuonesha kama wangemtii Mungu au la mpaka walipojaribiwa. Mungu alikuwa amewapa amri moja ndogo:

> “Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika” (Mwanzo 2:16,17).

### Adamu na Hawa walikuwa na uchaguzi

Wangeweza kumtii Mungu, au kutomtii na kula tunda la mti uliokatazwa. Walikuwa huru kuchagua. Mungu hakuwa ametengeneza watu walio kama mashine; wasioweza kuchagua kama watii au wasitii. Mungu alitaka wawe watu wanaoweza kuichagua njia yake kwa sababu ya kumpenda na kumheshimu.

Nyoka alikuja na kuwadanganya. Nyoka aliwaambia kuwa wasingekufa kama wangekula tunda lililokatazwa, na kwamba badala yake wangekuwa kama Mungu, wakijua mema na mabaya. Adamu na Hawa walitaka kuerevuka; kufanana zaidi na malaika. Walichagua kulila hilo tunda, na kwa kufanya hivyo walifanya dhambi kwa kutomtii Mungu.

### Adhabu

Mungu alikuwa amewaambia wangekufa kama wasingemtii. Kwa hiyo Adamu na Hawa walihukumiwa kifo, na kutimuliwa watoke katika bustani ya Edeni. Ingawa waliishi maisha marefu baada ya hapo, walibadilika na kuwa viumbe vinavyokufa. Walikuwa sasa wakichoka, wakiugua, wakizeeka na hatimaye kufa, kama ilivyo sasa kwako na kwangu.

### Kifo ni nini?

Kifo kilikuwa ni adhabu kwa sababu ya dhambi. Mungu alikuwa amesema:

> “U mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi” (Mwanzo 3:19).

Kwa hiyo mwili wa Adamu ulioza alipokufa na aliyarudia mavumbi, ambayo ndiyo yaliyokuwa yametumika kuufanya mwili wake. Mavumbi ni udongo. Mungu alimuumba Adamu kutokana na udongo wa nchi, na baada ya hapo alimpulizia pumzi ya uhai, kabla hajawa ‘nafsi hai’:

VUMBI + PUMZI YA UHAI = NAFSI HAI

Adamu alipokufa, ilikuwa ni:

NAFSI HAI – PUMZI YA UHAI = NAFSI ILIYOKUFA

Kwa hiyo tunaona kuwa:

NAFSI HAI ukitoa PUMZI YA UHAI ni VUMBI (udongo)

Hakuna sehemu ya Adamu iliyokwenda kuishi mbinguni alipokuwa amekufa; kwa hakika hakuna! Mauti yake yalikuwa ni adhabu ya Mungu kwa ajili ya dhambi, na kifo maana yake ilikuwa ni mwisho wa kuishi; mwisho wa uhai wote. Kifo cha Adamu hakikuwa kiwe na utofauti wowote na chetu. Sisi wote tunafanya dhambi, kwa hiyo sote tunakufa:

> “Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi” (Warumi 5:12).

Hili halina maana kwamba watu wote ni wauaji au wazinzi au waongo. Mawazo yasiyo ya wema, yenye ubaya: kiburi, choyo, hasira n.k (ambayo ni udhaifu wetu wote wa kila siku), yote ni dhambi machoni pa Mungu. Hakuna kati yetu atakayekwenda mbinguni tukifa.

**Hakuna chochote kinachoitwa ‘roho’ kisichokufa**

Hakuna mahali ambapo Biblia inataja uwepo wa ‘roho’ isiyokufa. Hili lina maana ya kwamba, hakuna kitu kinachoendelea kuishi mtu anapokuwa amekufa. Hakuna cheche ya uhai ya kimbingu isiyozimika katika mwanadamu anapokufa.

**‘Roho’ ni uhai: kiumbe hai, mtu, nafsi**

Ifuatayo ni orodha ya baadhi ya vifungu vilivyopo katika Biblia, vinavyoonesha sehemu neno hili ‘roho’ linapotumika. Hebu uvitazame mwenyewe, uone kama utakubaliana na maoni yaliyotolewa:

| REJEA | MAONI |
|---|---|
| Mwanzo 46:15 | Wana wa Yakobo (wanaoishi) wanaitwa ‘nafsi’ **(kwa Kingereza-souls)**; lenye maana ya ‘roho’. |
| Mwanzo 46:26 | “Nafsi zote” (all souls) hapa kwa hakika inamaanisha “watu wote”. |
| Walawi 5:2 | “Kama mtu akigusa kitu kilicho najisi …..” -neno ‘roho’ (soul) hapa ndilo lililotafsiriwa ‘mtu’. |
| Walawi 17:12 | “Kama mtu akifanya dhambi, na …..” (ms. 17): Neno ‘roho’ (soul) hapa ndilo lililotafsiriwa ‘mtu’. |
| | Maana ya roho ni **mtu**. Roho (souls) zinaweza kufanya dhambi, kwa maneno mengine **watu** wanaweza kufanya dhambi. “…….Hapana mtu mingoni mwenu aliye na ruhusa kula damu…..” (ms. 12). |
| Yoshua 10:28, 30,32, 35, 37 | Neno ‘roho’ (soul) hapa ndilo lililotafsiriwa ‘mtu’. |

| | |
|---|---|
| Yoshua 11:11<br><br>Matendo 27:37 | Hapana <u>mtu</u> ('roho' yaani mtu) kati yao aliyekuwa akiruhusiwa kula damu.<br><br>Neno <u>wote</u> katika mistari hiyo limekaa badala ya Roho: '<u>roho</u> wote pia' (All the souls).<br><br>'Roho wote' (yaani, watu wote) waliangamizwa kabisa. ('Roho' wanaweza kuangamizwa; kuuwawa!)<br><br>Neno 'wote' tena ni neno 'roho'.<br>"Wao wakawapiga <u>wote</u> pia waliokuwamo…."<br>(And they smote <u>all the souls</u> that were…..)<br><br>Waliwaua roho wote (watu wote); hakuna aliyebaki akipumua.<br><br>"Na sisi tuliokuwa ndani ya merikebu tulipata <u>watu</u> 276".<br>Neno 'watu' hapa ni neno 'roho'.<br>Roho 276 ni watu 276.<br>("And we were in all in the ship 276 <u>souls</u>")<br>Roho hapa ni wazi ni hao abiria. |

Kuna mifano mingi zaidi tungeweza kutoa kuonesha kuwa neno 'roho' maana yake ni mtu (au kiumbe hai). Waliotafsiri kwenye Kiswahili, kwa vyovyote walishakuwa na namna zao za kuamini, walichofanya tu ilikuwa kuweka vile walivyoona. Utata unaondoka kama tunaweza kulinganisha na Kingereza, ingawa nacho kina machapisho mengi-mengi.

Neno 'Roho' katika Kiebrania ni neno pia linalotumika kuhusiana na wanyama. Hili, bila shaka, linatusaidia kulielewa vizuri zaidi Kimaandiko. Kwenye Mwanzo 1:21, 24, 2:19 ni neno lililotafsiriwa 'kiumbe hai' kwenye Kiswahili. Kwenye Kingereza ni 'living creature'. Yote haya yanathibitisha kile kinachosemwa katika Mhubiri:

> "Kwa maana linalowatukia wanadamu linawatukia wanyama, jambo moja lawatukia; anavyokufa huyu ndivyo anavyokufa huyu, naam, wote wanayo pumzi moja; wala mwanadamu hana kitu cha kumpita mnyama; kwa maana yote ni ubatili. Wote huenda mahali pamoja, wote hutoka katika mavumbi, na hata mavumbini hurudi tena" (Mhu. 3:19, 20).

Hakuna utofauti wowote kati ya mtu na mnyama katika mauti. Mnyama hana sehemu inayokwenda mbinguni anapokufa, na mwanadamu ni hivyo hivyo. Wote wanakuwa ni miili isiyokuwa na uhai wanapoacha kupumua; inaoza, inakuwa udongo:

| "Roho": uhai, mtu, kiumbe hai |
|---|

Vifungu hivi vinatuonesha kinachotokea tunapokufa:

| | |
|---|---|
| Zaburi 146:4<br>Mhubiri 9:5<br>Zaburi 6:5<br>Zaburi 39:13<br>Zaburi 115:17 | "Pumzi yake hutoka, huurudia udongo wake, siku hiyo mawazo yake yapotea".<br>"Wafu hawajui neno lolote………"<br>"Mautini hapana kumbukumbu lako, katika kuzimu (kaburi) ni nani atakayekushukuru?"<br>"Uniachilie nikunjuke uso, kabla sijaondoka nisiwepo tena".<br>"Sio wafu wamsifuo BWANA, wala wowote washukao |

| | kwenye kimya” (kaburini). |
|---|---|

Vifungu hivi vyote vinaonesha kuwa, watu waliokufa hawana utambuzi wowote; hawawezi kufikiri.

Mfalme Hezekia alipoambiwa kuwa alikuwa afe, alisononeka sana. Alitaka aendelee kuishi kwa kuwa alijua kwenye mauti hakukuwa na kitu. Alimwomba Mungu aishi, ili aweze kuendelea kumsifu:

> “Kwa kuwa kuzimu hakuwezi kukusifu; mauti haiwezi kukuadhimisha; wale washukao shimoni hawawezi kuitarajia kweli yako” (Isaya 38:18).

Badala yake, anamwambia Mungu: “Aliye hai, naam, aliye hai, ndiye atakayekusifu, kama mimi leo” (ms.19).

**Je, mfalme Daudi?** Tunaambiwa wazi mfalme Daudi hakwenda mbinguni, ingawa anaitwa mtu aliyekuwa na moyo uliompendeza sana Mungu (Matendo 2:34, 13:22)

Watu wote tupo kwenye hukumu ya kifo kwa sababu ya dhambi. Hakuna anayeendelea kuishi kwa namna yoyote nyingine baada ya kufa.

Kama hatulielewi hili vizuri, hatuwezi kamwe kutambua jinsi ambavyo Bwana Yesu alivyoteseka na kufa ili kutuweka huru na dhambi, na matokeo yake.

Kama tungekuwa na ‘roho zisizokufa’, kusingekuwa na haja ya Yesu kutufia. Biblia inatuambia, hakuna tumaini la uzima kama sio katika Kristo.

**Muhtasari**

1. Mungu alimuumba Adamu kutokana na mavumbi ya nchi.
2. Alimfanya aweze kuishi kwa kumpulizia pumzi ya uhai katika pua zake.
3. Mungu alimpa Adamu amri. Alimwambia kwamba kama akiivunja amri yake, adhabu yake itakuwa kifo.
4. Adamu na Hawa hawakumtii Mungu; waliivunja amri yake. Matokeo yake wakawa viumbe vinavyokufa.
5. Watu wote wanatokana na Adamu, na wanairithi hulka yake ya dhambi. Watu wote wanakosa na wanakufa.
6. Neno ‘roho’ linamaanisha uhai au kuwa hai, na kwa kawaida linatumika kwa mtu.
7. Msemo ‘roho isiyokufa’ haupo kwenye Biblia.
8. Kifo ni adhabu na matokeo ya dhambi (sio ‘Mungu kumpenda anayekufa zaidi’!).
9. Hakuna sehemu ndani yetu au kitu kinachoendelea kuishi tunapokufa.

**Kifungu cha kusoma**: Mhubiri 9

**Msitari wa kushika**: Zaburi 146:4
“(Mtu anapokuwa akifa)Pumzi yake hutoka, huurudia udongo wake, siku hiyo mawazo yake yapotea”.